# Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili

Fabiola Hassan

**Ikisiri**

Makala hii inahusu upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Lengo lake ni kubainisha aina za upinduzi wa kimahali, vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu utokeaji wa mchakato huo, pamoja na vimahali vinavyoweza na vile visivyoweza kupinduliwa katika tungo. Data zimekusanywa kwa mbinu ya upitiaji wa nyaraka na usaili. Ufafanuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu (SLA) ya Bresnan na Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Makala inabainisha kwamba, tofauti na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kichewa (N31, Malawi) au Kizulu (S40, Afrika ya Kusini) ambazo zina upinduzi wa kimahali wa kimofolojia au wa kisemantiki, lugha ya Kiswahili ina aina mbili za upinduzi wa kimahali. Upinduzi huo hutokea iwapo muundo wa kitenzi kinachounda tungo una kithimu[1] na kimahali[2]. Aidha, tofauti na lugha nyingine za Kibantu, kama vile Kiswana (S31, Botswana), katika lugha ya Kiswahili kitenzi ambacho muundo wake una mtenda hakiruhusu upinduzi wa kimahali. Vilevile, vimahali vinavyoweza kupinduliwa ni vijalizo. Kwa upande mwingine, vimahali visivyoweza kupinduliwa ni chagizo. Makala inahitimisha kwamba lugha ya Kiswahili inafanana na kutofautiana na lugha nyingine za Kibantu katika udhihirishaji wa upinduzi wa kimahali.

## 1.0 Utangulizi

Upinduzi wa kimahali ni mchakato ambao neno au kirai kinachorejelea mahali (kimahali), ambacho kwa kawaida hutokea baada ya kitenzi, hupandishwa hadhi na kuhamishiwa kabla ya kitenzi katika nafasi ya kiima. Wakati huohuo, neno au kirai kinachorejelea kitu kinachohusishwa na mahali (kithimu), ambacho kwa kawaida

[1] Istilahi ‘kithimu’ imetumika kwa maana mbili kama ifuatavyo: Mosi, kithimu ni neno au kirai kinachorejelea mtu/kiumbe/kitu kinachohusishwa na mahali au kinachoonesha mabadiliko ya mahali kwa kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Pili, kithimu ni dhima ya kisemantiki ambayo inawakilishwa na neno au kirai kinachohusishwa na mahali au kinachoonesha mabadiliko ya mahali katika tungo.

[2] Istilahi ‘kimahali’ imetumika kwa maana mbili kama ifuatavyo: Mosi, kimahali ni neno au kirai kinachorejelea mahali katika tungo. Pili, kimahali ni dhima ya kisemantiki ambayo inawakilishwa na neno au kirai kinachorejelea mahali katika tungo.

hutokea kabla ya kitenzi katika nafasi ya kiima, hushushwa hadhi na kuhamishiwa baada ya kitenzi katika nafasi ya yambwa. Mfano wa (1) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (1). | a) | ***Maji*** | *ya-me-ja-a* | ***m-to-ni*** |
| | | kng6.maji | kk6-tmlf-ja-kt | kng3-to-KTM |
| | | 'Maji yamejaa mtoni.' | | |
| | b) | ***M-to-ni*** | *ku-me-ja-a* | ***maji*** |
| | | Kng3-to-ktm | kk17-tmlf-ja-kt | kng6.maji |
| | | 'Mtoni kumejaa maji.' | | |

Mfano wa 1(a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kithimu ni *maji* na kimahali ni *mtoni*. Kithimu kimetokea kabla ya kitenzi *yamejaa* na kimahali kimetokea baada ya kitenzi hicho. Mfano wa 1(b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kimahali *mtoni* kimetokea katika nafasi ya kiima kabla ya kitenzi *kumejaa*. Aidha, kithimu *maji* kimetokea baada ya kitenzi hicho katika nafasi ya yambwa.

Kiima ni dhima ya kisarufi inayofanywa na neno au kirai ambacho kwa kawaida hutokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya kitenzi. Neno au kirai hicho kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi. Mathalani, katika mfano wa (1b), kimahali *mtoni* ni kiima kwa sababu kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli 17 *ku-*. Yambwa ni dhima ya kisarufi inayofanywa na neno au kirai ambacho kinatokea mara baada ya kitenzi. Mathalani, katika mfano wa (1b), kithimu *maji* ni yambwa kwa sababu kimetokea baada ya kitenzi.

Katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Kichewa (N31, Malawi), maneno yanayorejelea mahali huambikwa viambishi vya ngeli za mahali 16 **pa-*, 17 **ku-*, au 18 **mu-* mwanzoni mwa mashina yake (mfano, Kichewa; ***ku****mudzi* 'kijijini'). Katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Kikuyu (E51, Kenya), maneno hayo huambikwa kiambishi tamati cha mahali *–ni* au *ng* mwishoni mwa mashina yake. Polome (1967), Mkude (2005), Amidu (2007) na Mpiranya (2015) wanakubaliana kuwa, katika Kiswahili, maneno yanayorejelea mahali huambikwa kiambishi tamati cha mahali *-ni* (mfano, *darasa****ni***). Vilevile, huweza kuambatana na kihusishi cha mahali (mfano, ***juu ya*** *meza*). Naye Buberwa (2016) anaeleza kuwa, katika Kiswahili, majina mengi ya mahali hayaambikwi kiambishi tamati cha mahali *-ni* (mfano, *Dodoma*).

Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu upinduzi wa kimahali katika lugha za Kibantu. Mathalani, Bresnan na Kanerva (1989) na Bresnan (1994) katika Kichewa (N31, Malawi); Demuth na Mmusi (1997) katika Kiswana (S31, Botswana); Salzman (2004) katika Kichewa (N31, Malawi), Kisotho (S33, Afrika ya Kusini), Kishona (S10, Zimbabwe), Kiswana (S31, Botswana), Kinyarwanda (DJ61, Rwanda), Kirundi (DJ62, Burundi) na Kichaga (E621, Tanzania); Marten (2006) katika Kiotijiherero (R31, Herero); Buel (2007) katika Kizulu (S40, Afrika

Kusini) na Kitharaka (E54, Kenya); Diercks (2009) katika Kilubukusu (J30, Kenya Mashariki); Creissels (2011) katika Kiswana (S31, Botswana); Zeller (2013) katika Kizulu (S40, Afrika ya Kusini); na Guerois (2016) katika Kimakhuwa (P31, Tanzania) na Kichuwabo (P34, Msumbiji). Katika tafiti zao, pamoja na mambo mengine, wanajadili kuhusu aina za upinduzi wa kimahali, vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu utokeaji wa upinduzi huo, pamoja na vimahali vinavyoweza na vile visivyoweza kupinduliwa. Kutokana na tafiti hizo, imebainika kwamba, utokeaji wa ruwaza hizo hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Aidha, hitimisho lililofikiwa kuhusu aina za upinduzi wa kimahali zinazojidhihirisha katika lugha moja ni suala linalohitaji kuchunguzwa vizuri. Mathalani, Buel (2007) anahitimisha kwamba katika lugha moja kuna ama upinduzi wa kimahali wa kimofolojia au wa kisemantiki. Anahoji uwezekano wa lugha moja kuwa na upinduzi wa kimahali wa aina zote mbili. Kwa ujumla, masuala haya yamechochea hamu ya kufanya utafiti uliozaa makala hii.

Makala hii inahusu upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili (G42, Tanzania). Licha ya kuwapo kwa lahaja mbalimbali, makala hii inahusu data za Kiswahili sanifu. Lengo la makala hii ni kubainisha aina za upinduzi wa kimahali, vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu utokeaji wa mchakato huo, pamoja na vimahali vinavyoweza na vile visivyoweza kupinduliwa. Baadhi ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili wamegusia mchakato huo bila kuonesha mfungamano uliopo baina ya masuala hayo (taz. Mkude, 2005; Marten, 2013; na Marten na Van der Wal, 2014). Data zimekusanywa kwa mbinu ya upitiaji wa nyaraka na usaili. Mtafiti alisoma matini mbalimbali (Ashton, 1947: 125-130; Mkude, 2005:153-155; Khamis, 2008: 9-214). Katika matini hizo aliweza kukusanya tungo mbalimbali zenye upinduzi wa kimahali. Katika usaili, mtafiti aliandaa tungo zinazohusiana na upinduzi wa kimahali; aliwaomba watoa taarifa kueleza kama tungo hizo zinakubalika au hazikubaliki. Mbinu hizi zilisaidia kupata data kulingana na malengo ya makala hii. Mbinu ya usaili ilitumika kwa wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Data zimefafanuliwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya SLA. Makala ina sehemu tano ambazo ni utangulizi, ufafanuzi wa upinduzi wa kimahali kwa ujumla, Nadharia ya SLA, upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili, pamoja na hitimisho.

## 2.0 Upinduzi wa Kimahali

Wanaisimu mbalimbali wamefafanua aina za upinduzi wa kimahali katika lugha za Kibantu. Mathalani, Buel (2007) anaeleza kuwa kuna aina mbili za upinduzi wa kimahali. Aina hizo ni upinduzi wa kimahali wa kimofolojia na upinduzi wa kimahali wa kisemantiki. Katika aina ya kwanza, kimahali chenye kiambishi cha ngeli ya mahali, au kiambishi tamati cha mahali, au kihusishi cha mahali hutokea kabla ya kitenzi. Kimahali hicho kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya mahali 16 **pa*-, 17 **ku*-, au 18 **mu*- kama ilivyo katika mfano wa (1b). Katika aina ya pili, kimahali cha kisemantiki (ambacho hakina kiashiria chochote cha kimofolojia cha umahali) hutokea kabla ya kitenzi. Kimahali hicho kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi

ambacho siyo cha ngeli ya mahali kama inavyoonekana katika mfano wa (2b) wa lugha ya Kitharaka (E54, Kenya).

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (2) | a) | *Aba-ntu* | *aba-dala* | *ba- hlala* | ***zilezi*** | ***zi-ndlu*** |
| | | kng2-watu | kv2-wazee | kk2-ishi | kng10.hizi | kng10-nyumba |
| | | 'Watu wazee wanaishi katika nyumba hizi.' | | | | |
| | b) | ***Zilezi*** | ***zi-ndlu*** | ***zi**-hlala* | *aba-ntu* | *aba-dala* |
| | | kng10.hizi | kng10-nyumba | kk10-ishi | kng2-watu | kv2-wazee |
| | | 'Nyumba hizi zinaishi watu wazee.' | | | | |
| | | (Katika nyumba hizi mnaishi watu wazee.) | | | | |
| | | **Chanzo**: Buel (2007: 108) | | | | |

Katika mfano wa (2b), kimahali *zilezi zindlu* 'nyumba hizi' kinatokea kabla ya kitenzi *zihlala* 'zinaishi'. Kimahali hiki hakijaambikwa kiambishi cha ngeli ya mahali bali kimeambikwa kiambishi cha ngeli ya 10 *zi*- ambacho kinaonesha upatanishi wa kisarufi na kitenzi *zihlala* 'zinaishi'. Licha ya kutoambikwa kiambishi cha ngeli ya mahali, kimahali *zilezi zindlu* 'nyumba hizi' kinarejelea umahali. Hivyo, aina za upinduzi wa kimahali hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Kwa mfano, lugha ya Kichewa (N31, Malawi), ina upinduzi wa kimahali wa kimofolojia, wakati lugha ya Kitharaka (E54, Kenya) ina upinduzi wa kimahali wa kisemantiki.

Aidha, vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu utokeaji wa upinduzi wa kimahali hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Mathalani, Bresnan na Kanerva (1989) na Bresnan (1994) wanaeleza kuwa, katika Kichewa (N31, Malawi), kitenzi ambacho muundo wake una kithimu na kimahali huruhusu upinduzi wa kimahali. Kwa upande mwingine, kitenzi ambacho muundo wake una mtenda[3] hakiruhusu upinduzi huo. Tofauti na Kichewa (N31, Malawi), Demuth na Mmusi (1997) wanaeleza kuwa, katika Kiswana (S31, Botswana) kitenzi ambacho muundo wake una mtenda kinaruhusu upinduzi huo ilimradi tu muundo huo usiwe na mtenda na kithimu kwa wakati mmoja. Hivyo, ni dhahiri kwamba vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu upinduzi wa kimahali hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine.

Vilevile, kuna ufafanuzi kuhusu vimahali vinavyoweza na vile visivyoweza kupinduliwa. Mathalani, Bresnan (1994: 82-83) anaeleza kwamba katika Kichewa (N31), kimahali kinachopinduliwa lazima kiwe ni kipashio cha lazima (kijalizo). Kwa upande mwingine, kimahali kisichoweza kupinduliwa ni kimahali ambacho siyo kipashio cha lazima (chagizo). Hata hivyo, Bresnan (1994: 84-85) anaeleza kuwa wakati mwingine kuna ugumu wa kubainisha suala hili. Tukifuata mawazo ya Dowty (2000: 1-2), kisemantiki, kijalizo ni kipashio kinachokamilisha maana katika tungo. Kisintaksia, kijalizo ni kipashio cha lazima kwa sababu hakiwezi kuondolewa bila kuleta athari ya kisarufi katika tungo. Vilevile, kama TUKI

[3] Mtenda ni dhima ya kisemantiki inayorejelea mfanyaji au mwanzilishi wa kitendo.

(1990: 3) wanavyofafanua, chagizo ni kipashio kinachotumika kama nyongeza ya maana, na ambacho kinaweza kuondolewa na bado sentensi ikabaki na maana ya msingi. Mfano wa (3a) unaonesha kimahali ambacho ni kijalizo cha kitenzi na mfano wa (3b) ni kimahali ambacho ni kijalizo kilichotokana na uambikaji wa kiambishi cha utendea mtawalia. Mfano wa (4) unaonesha kimahali ambacho ni chagizo.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (3) | a) | *Ugonjwa* | *u-me-ene-a* | ***m-ji-ni*** | |
| | | kng14-gonjwa | kk14-knj-ene-kt | kng3-mz-ktm | |
| | | 'Ugonjwa umeenea mjini.' | | | |
| | b) | *Juma* | *a-na-som-e-a* | *ki-tabu* | ***meza-ni*** |
| | | Kng1.Juma | kk1-nj-som-ktnda-kt | kng7-tabu | kng9.meza-ktm |
| | | 'Juma anasomea kitabu mezani.' | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (4) | *M-toto* | *a-na-chek-a* | ***chumba-ni*** |
| | kng1-toto | kk1-knj-chek-kt | kng7-chumba-ktm |
| | 'Mtoto anacheka chumbani.' | | |

Vimahali *mjini* na *mezani* katika mifano (3a) na (3b) ni vijalizo kwa sababu ni vipashio vya lazima katika tungo hizo. Kimahali *chumbani* katika (4) ni chagizo kwa sababu siyo kipashio cha lazima katika tungo hiyo.

## 3.0 Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu (SLA)

SLA ni nadharia iliyoasisiwa na Joan Bresnan na Ronald Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Nadharia hii inazingatia ufafanuzi wa vipengele vya lugha kwa kutumia taarifa za kileksika na uamilifu wa viambajengo vya sentensi. Vilevile, inahusisha miundo mbalimbali ya sentensi kwa kutumia kanuni. Miundo hiyo ni muundo amilifu (MAM) ambao unaonesha dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi pamoja na sifa za kimofosintaksia za viambajengo hivyo. Dhima hizo za kisarufi ni kiima, yambwa, yambwa$_{\theta}$, oblikyu[4], kijalizo, na chagizo. Dhima hizi zinaashiriwa na sifa za kimofolojia, kisintaksia, na kisemantiki katika lugha za Kibantu. Mathalani, kiima kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kipatanishi cha kiima. Yambwa ina sifa ya kuwekewa kiambishi yambwa katika kitenzi au kuwa kiima cha sentensi tendwa. Pia, kuna muundo wa vishiriki

[4] Oblikyu$_{ø}$ ni istilahi iliyotoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza "Oblique$_{ø}$". Istilahi hii ina maana ya dhima ya kisarufi inayofanywa na neno au kirai kinachohusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki (mathalani, umahali). Pia, neno au kirai hicho hakina sifa za uyambwa katika tungo. Katika lugha za Kibantu, kimahali kinahusishwa na dhima hii. Katika makala hii dhima hii inajulikana pia kama oblikyu$_{\text{kimahali}}$.

vya kitenzi (MVSH) ambao unaonesha idadi na dhima za kisemantiki za vishiriki vya kitenzi. Muundo huu unaonesha idadi ya vishiriki katika kitenzi na dhima zake kisemantiki. Dhima za kisemantiki ni kama vile mtenda, kithimu na kimahali. Mathalani, kitenzi *weka* kinahitaji vishiriki vitatu ambavyo ni mwekaji (mtenda), kinachowekwa (kithimu), na mahali (kimahali). Kwa hiyo, MVSH wa kitenzi *weka* ni <mtenda, kithimu, kimahali>.

Dhima za kisemantiki zinahusishwa na dhima za kisarufi kwa kuzingatia masuala matano. Kwanza, ***udarajia wa dhima za kisemantiki***, yaani mpangilio wa dhima za kisemantiki kulingana na uwezo wa dhima husika kuwa kiima kuliko nyingine. Mathalani, Mkude (2005) anapendekeza udarajia wa dhima za kisemantiki katika Kiswahili kuwa ni: *Mtenda=>Eksiperiensa=>Mpokeaji=>Mnufaika=>Kithimu=>Kiathirika=>Kimahali=>Kifaa.* Kwa kuzingatia udarajia huu, dhima ya kisemantiki iliyopo katika nafasi ya juu ndiyo inaweza kuwa kiima kuliko ile iliyopo katika nafasi ya chini. Mathalani, kithimu kinapaswa kuwa kiima na siyo kimahali. Hata hivyo, kuna wakati kimahali ambacho kipo katika nafasi ya chini kinapandishwa hadhi na kuwa kiima licha ya kuwapo kwa kithimu. Upandishwaji wa hadhi ya kimahali hutokea iwapo kimahali ni mada katika sentensi. Pili, ni ***ufafanuzi wa dhima za kisarufi*** kwa kutumia sifa bainifu. Hivyo, kwa mujibu wa SLA, kiima ni dhima inayofanywa na neno au kirai kisichohusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki; pia hakina sifa za uyambwa [-h, -y]. Yambwa ni dhima inayofanywa na neno au kirai kisichohusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki; lakini kina sifa za uyambwa [-h, +y]. Yambwa$_{\theta}$ ni dhima inayofanywa na neno au kirai kinachohusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki; pia kina sifa za uyambwa [+h, +y]. Oblikyu$_{\theta}$ ni dhima inayofanywa na neno au kirai kinachohusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki; lakini hakina sifa za uyambwa [+h, -y]. Tatu, ni ***kanuni ya uhusishaji kimajumui*** ambapo mtenda anahusishwa na sifa ya [-y] na hivyo anaweza kuwa kiima au oblikyu$_{\theta}$, kithimu kinahusishwa na sifa ya [-h] na hivyo kinaweza kuwa kiima au yambwa, na kimahali kinahusishwa na sifa ya [-y] na hivyo kinaweza kuwa kiima au oblikyu$_{\theta}$ kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (1). Nne, ni ***michakato ya kimofolojia*** ambayo inaongeza au kupunguza idadi ya vishiriki vya kitenzi. Michakato hiyo ni kama vile uambikaji wa kiambishi cha utendea au utendwa. Michakato hii inasababisha kufanyika kwa miundo ya vitenzi vinavyokubali upinduzi wa kimahali. Tano, ni ***sharti la ukubalifu*** ambalo lina kanuni ndogo mbili. Kanuni ya *kiima* inayohitaji kwamba kila tungo lazima iwe na kiima na kanuni ya *uwiano-dhima* inayohitaji kwamba kila dhima moja ya kisemantiki ihusishwe na dhima moja ya kisarufi na kinyume chake.

**Kielelezo Na. 1: Uhusishaji wa Kimajumui wa Dhima za Kisemantiki na za Kisarufi**

| | | |
|---|---|---|
| Mtenda | Kithimu | Kimahali |
| ↓ | ↓ | ↓ |
| [-y] | [-n] | [-y] |
| Kiima/Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ | Kiima/Yambwa | |
| Kiima/Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ | | |

Kwa ujumla, misingi ya Nadharia ya SLA imesaidia katika ufafanuzi wa data kulingana na malengo ya makala hii.

### 4.0 Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ina tungo zenye upinduzi wa kimahali. Tungo hizo hutokea iwapo kimahali ni mada[5] katika tungo. Kwa sababu kimahali ni mada, basi hupandishwa hadhi na kutokea mwanzoni mwa sentensi katika nafasi ya kiima. Katika sehemu 4.1, 4.2 na 4.3, tumebainisha aina za upinduzi wa kimahali, vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu utokeaji wa upinduzi wa kimahali, pamoja na vimahali vinavyoweza na vile visivyoweza kupinduliwa katika tungo.

### 4.1 Aina za Upinduzi wa Kimahali

Katika lugha ya Kiswahili kuna aina mbili za upinduzi wa kimahali. Aina ya kwanza ni upinduzi wa kimahali wa kimofolojia. Katika tungo zenye upinduzi huo, kimahali ambacho kina kiambishi tamati cha umahali *-ni* au kihusishi cha mahali hutokea kabla ya kitenzi. Kimahali hicho kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya mahali 16 *pa-*, 17 *ku-*, au 18 *mu-* kama inavyoonekana katika mfano wa (5b) na (6b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (5) | a) | *Maji* | *ya-me-kauk-a* | ***m-to-ni*** |
| | | kng6.maji | kk6-knj-kauk-kt | kng3-mz-ktm |

'Maji yamekauka mtoni.'

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | b) | ***M-to-ni*** | ***ku***-*me-kauk-a* | *maji* |
| | | kng3-mz-ktm | kk17-knj-kauk-kt | kng6.maji |

'Mtoni kumejaa maji.'
(Khamis, 2008: 143)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (6) | a) | *M-dudu* | *a-me-ingi-a* | ***katika*** | ***ch-umba*** | ***ch-angu*** |
| | | kng1-dudu | Kk1-knj-ingi-kt | katika | kng7-umba | kv7-angu |

[5] Mada ni taarifa ambayo inaeleza kuwa sentensi inahusu nini. Katika lugha za Kibantu, mara nyingi taarifa hii inawakilishwa na kiima cha sentensi.

'Mdudu ameingia katika chumba changu.'

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| b) | ***Katika*** | ***ch-umba*** | ***ch-angu*** | *m-me-ingi-a* | *m-dudu* |
| | katika | kng7-umba | kv7-angu | Kk18-knj-ingi-kt | kng1-dudu |

'Katika chumba changu mmeingia mdudu.'

Mfano wa (5b) unaonesha kuwa kimahali cha kimofolojia *mtoni* kimetokea kabla ya kitenzi *kumekauka*. Kimahali hiki kina kiambishi tamati cha mahali *-ni* na kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya mahali 17 *ku*. Mfano wa (6b) unaonesha kuwa kimahali cha kimofolojia *katika chumba changu* kimetokea kabla ya kitenzi *mmeingia*. Kimahali hiki kina kihusishi cha mahali *katika* na kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya mahali 18 *m-*.

Aina ya pili ni upinduzi wa kimahali wa kisemantiki. Katika tungo zenye upinduzi huo, kimahali ambacho hakina kiambishi au kihusishi cha mahali kinatokea kabla ya kitenzi. Kimahali hicho kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli nyingine ambayo siyo ngeli ya mahali kama inavyoonekana katika mifano ya (7a) na (7b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (7) | a) | ***M-to*** | ***u**-me-kauk-a* | *maji* |
| | | kng3-mz | kk3-knj-kauk-kt | kng6.maji |

'Mto umekauka maji.'

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| b) | ***Ch-umba*** | ***ch-angu*** | ***ki**-me-ingi-a* | *m-dudu* |
| | kng7-umba | kv7-angu | Kk7-knj-ingi-kt | kng1-dudu |

'Chumba changu kimeingia mdudu.'

Mfano wa (7a) unaonesha kuwa nomino *mto* imetokea kabla ya kitenzi *umekauka*. Nomino hii haina kiambishi tamati cha umahali wala kihusishi cha mahali lakini inarejelea dhana ya umahali kisemantiki. Aidha, nomino hii inaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya 3 *u-*, kiambishi ambacho siyo cha ngeli ya mahali. Mfano wa (7b) unaonesha kuwa kirai *chumba changu* kimetokea kabla ya kitenzi *kimeingia*. Kirai hiki hakina kihusishi cha mahali ingawa kinarejelea dhana ya umahali kisemantiki. Aidha, kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya 7 *ki-*, kiambishi ambacho siyo cha ngeli ya mahali.

Aidha, imebainika kwamba tungo katika mifano ya (5b), (6b), (7a) na (7b) inaonesha mfanano wa sifa. Katika tungo zote, kimahali kinatokea kabla ya kitenzi na kithimu kinatokea baada ya kitenzi. Pia, kimahali kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia ama kiambishi cha ngeli ya mahali au cha ngeli isiyokuwa ya mahali. Vilevile, tungo hizo zimeundwa na kitenzi *kauka*/*ingia*. Miundo ya vitenzi hivi ina kithimu na kimahali. Kwa hiyo, aina zote mbili za upinduzi wa kimahali zinajidhihirisha katika lugha ya Kiswahili. Aidha, lugha hii

inatofautiana na lugha nyingine za Kibantu ambazo zina upinduzi wa kimahali wa aina moja. Mathalani, lugha ya Kichewa (N31) na Kiswana (S31) zina upinduzi wa kimahali unaojidhihirisha kimofolojia pekee. Kwa upande mwingine, Kizulu (S40) na Kitharaka (E54) ni lugha zenye upinduzi wa kimahali wa kisemantiki pekee.

### 4.2 Vitenzi Vinavyoruhusu na Vile Visivyoruhusu Utokeaji wa Upinduzi wa Kimahali

Vitenzi huweza kuainishwa kwa kutumia dhima za kisemantiki za vishiriki vyake. Licha ya kuwapo kwa tofauti ya idadi na istilahi, dhima za kisemantiki zinazotajwa mara nyingi ni mtenda, muathirika, kifaa, mnufaika, mpokeaji, kithimu na kimahali (Bresnan na Kanerva, 1989; Givon, 2001; Kroeger, 2004; na Mkude, 2005). Vitenzi vinavyohusika katika tungo zenye upinduzi wa kimahali ni vitenzi mahali. Kim (1999: 28) anaeleza kuwa kitenzi mahali ni kitenzi ambacho kinaonesha uhusiano baina ya kithimu na kimahali. Hivyo, kutokana na fasili ya Kim, muundo wa kitenzi mahali una kithimu na kimahali. Licha ya kithimu na kimahali, pia kuna vitenzi mahali ambavyo miundo yake ina mtenda. Kithimu ni dhima ya kisemantiki inayorejelea kitu kinachohusishwa na mahali au kinachoonesha mabadiliko ya mahali. Kimahali ni dhima ya kisemantiki inayorejelea mahali pa jumla, mahususi au ndani. Mtenda ni dhima ya kisemantiki inayorejelea mtendaji wa tendo. Kwa hiyo, kwa kuzingatia dhima za kisemantiki tunapata vitenzi vya aina mbalimbali. Mathalani, kitenzi chenye kithimu na kimahali, kitenzi chenye mtenda na kimahali, na kitenzi chenye mtenda, kithimu na kimahali. Kati ya vitenzi hivi, kuna vitenzi vinavyoruhusu na vingine haviruhusu utokeaji wa tungo yenye upinduzi wa kimahali kama ilivyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

#### 4.2.1 Vitenzi Vinavyoruhusu Utokeaji wa Upinduzi wa Kimahali

Imebainika kwamba vitenzi vinavyoruhusu upinduzi wa kimahali ni hivi vifuatavyo: Kwanza, kitenzi chenye muundo wa kithimu na kimahali. Pili, kitenzi chenye muundo wa mtenda, kithimu, na kimahali (tendwa).

##### 4.2.1.1 Kitenzi Chenye Muundo wa Kithimu na Kimahali

Hiki ni kitenzi ambacho muundo wake una kishiriki kinachohusishwa na mahali (kithimu) pamoja na kishiriki kinachorejelea mahali (kimahali). Kitenzi hiki kinaweza kuwa na sifa ya ujongezi au utuli.

**(a) Kitenzi Jongezi chenye Muundo wa Kithimu na Kimahali**

Hiki ni kitenzi ambacho muundo wake una kishiriki kinachohusishwa na mahali (kithimu) pamoja na kishiriki kinachorejelea mahali (kimahali). Kitenzi hiki kinaonesha uhusiano baina ya kitu kinachojongea na mahali. Mifano ya vitenzi hivi ni *ingia*, *toka*, *churuzika*, *tua*, *tumbukia*, *bubujika*, *pukutika* na *chomoka*. Vitenzi vyenye muundo huu vinaruhusu upinduzi wa kimahali kama inavyoonekana katika mfano wa (8b).

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (8) | a) | *M-dudu* | ***a-me-ingi-a*** | *katika* | *maji* |
| | | kng1-dudu | kk1-knj-ingi-kt | katika | kng6.maji |
| | | 'Mdudu ameingia katika maji.' | | | |
| | b) | *Maji* | ***ya-me-ingi-a*** | *m-dudu* | |
| | | kng6.maji | kk6-knj-ingi-kt | kng1-dudu | |
| | | 'Maji yameingia mdudu.' | | | |

Mfano wa (8a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Mfano wa (8b) unaonesha tungo yenye upinduzi. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *ingia,* ambacho muundo wake una kithimu *mdudu* na kimahali *katika maji/maji*. Kwa mujibu wa SLA, kithimu kinaweza kuwa kiima au yambwa, na kimahali kinaweza kuwa kiima au oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$. Katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali (8a), kwa kutumia kanuni ya kiima kwamba kila tungo lazima iwe na kiima, kithimu *mdudu* ni kiima. Hii ni kwa sababu, katika udarajia wa dhima za kisemantiki, kithimu kipo katika nafasi ya juu kuliko kimahali. Aidha, kimahali *katika maji* kinaweza kuwa kiima au oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$. Hata hivyo, kwa sababu kuna kiima na kwa kutumia kanuni ya uwiano-dhima kwamba kila dhima moja ya kisemantiki ihusishwe na dhima moja ya kisarufi na kinyume chake, kimahali hicho ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (2).

**Kielelezo Na. 2:** ***Mdudu ameingia katika maji***

| | | |
|---|---|---|
| | *ingia* <kithimu, kimahali> | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-y] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (2) kinaonesha kuwa, katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali yenye kitenzi chenye kithimu na kimahali, kithimu ni kiima na kimahali ni Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$.

Ingawa katika udarajia wa dhima za kisemantiki kimahali kipo katika nafasi ya chini kuliko kithimu, kimahali kinapandishwa hadhi na kuwa kiima. Mchakato huo hutokea iwapo kimahali ni mada katika sentensi. Kwa hiyo, kimahali cha kisemantiki *maji* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (3). Aidha, ikumbukwe kwamba kithimu kinaweza kuwa kiima au yambwa. Lakini kwa sababu kuna kiima na kwa kutumia kanuni ya uwiano-dhima kwamba kila dhima moja ya kisemantiki ihusishwe na dhima moja ya kisarufi na kinyume chake, kithimu *mdudu* kinashushwa hadhi na kuwa yambwa$_{\textbf{ø}}$. Kithimu hicho ni yambwa$_{\textbf{ø}}$ badala ya yambwa kwa sababu kinahusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki ambayo ni kithimu. Pia, licha ya kuwa katika nafasi ya yambwa na kuonesha mfungamano wa kimatamshi na kitenzi, hakiwezi kuwekewa kiambishi yambwa katika kitenzi na maana

ikarejelea dhana ya awali kuwa *mdudu* ndiye aliyeingia *katika maji*. Iwapo kinawekewa kiambishi yambwa (**maji yame**mu**ingia* ***mdudu***), maana inayojitokeza ni kwamba *maji* ndiyo yaliyomuingia *mdudu*. Vilevile, hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa bila kubadili maana kwamba *mdudu* ndiye aliyeingia *katika maji*. Iwapo kinalazimishwa na kuwa kiima cha sentensi tendwa (*****mdudu*** *ameingi**wa** na maji*) maana inayochanuzwa na sentensi tendwa ni kwamba *maji* ndiyo yaliyomuingia *mdudu*.

**Kielelezo Na. 3:** ***Maji yameingia mdudu***

| | | |
|---|---|---|
| | *ingia* <kithimu, kimahali> | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui: | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima: | | [-h] |
| | Yambwa$_{ø}$ | Kiima |

Kielelezo Na. (3) kinaonesha kuwa kitenzi *ingia* <kithimu, kimahali> kinaruhusu utokeaji wa tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hiyo, kimahali ni kiima na kithimu ni yambwa$_{ø}$. Lugha ya Kiswahili inafanana na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kitharaka (E54, Kenya). Katika lugha hiyo, kitenzi chenye muundo huu kinaruhusu upinduzi wa kimahali. Kwa upande mwingine, inatofautiana na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kizulu (S40, Afrika ya Kusini). Katika lugha hiyo, kitenzi chenye muundo huu hakiruhusu utokeaji wa tungo yenye upinduzi wa kimahali.

**(b) Kitenzi Tuli chenye Muundo wa Kithimu na Kimahali**

Hiki ni kitenzi mahali ambacho muundo wake una kithimu pamoja na kimahali. Kitenzi hiki, kinaonesha uhusiano baina ya kitu kisichojongea na mahali. Mifano ya vitenzi hivi ni *ng'aa*, *nuka*, *tanda*, *zagaa*, *enea*, *jaa*, *tapakaa* na *sambaa*. Vitenzi hivi vinaruhusu upinduzi wa kimahali kama inavyoonekana katika mfano wa (9b).

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (9) | a) | *Wingu* | zito | ***li-me-tand-a*** | *anga-ni* |
| | | kng5.wingu | kv5.zito | kk5-knj-tanda-kt | kng5.anga-ktm |
| | | 'Wingu zito limetanda angani.' | | | |
| | b) | *Anga-ni* | ***ku-me-tand-a*** | *wingu* | zito |
| | | kng5.anga-ktm | kk17-knj-tanda-kt | kng5.wingu | kv5.zito |
| | | 'Angani kumetanda wingu zito.' | | | |

Mfano wa (9a) unaonesha tungo isiyo ya upinduzi wa kimahali. Mfano wa (9b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *tanda*. Muundo wa kitenzi hiki una kithimu *wingu zito* pamoja na kimahali *angani*.

Katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali (9a), kwa kutumia kanuni ya kiima kwamba kila tungo lazima iwe na kiima, kithimu *wingu* zito ni kiima kwa sababu kipo katika nafasi ya juu kuliko kimahali katika udarajia wa dhima za

kisemantiki. Kwa sababu kuna kiima na kwa kutumia kanuni ya uwiano-dhima, kimahali hicho kinahusishwa na dhima ya oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (4).

**Kielelezo Na. 4:** ***Wingu zito limetanda angani***

| | | |
|---|---|---|
| | *tanda* <kithimu kimahali> | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-y] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (4) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *tanda*, kithimu ni kiima na kimahali ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$.

Kitenzi *tanda* kinaruhusu utokeaji wa tungo yenye upinduzi wa kimahali (9b). Katika tungo hiyo, kimahali *angani* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima. Aidha, ikumbukwe kuwa kithimu *wingu zito* kinaweza kuwa kiima au yambwa. Kwa sababu kuna kiima, na kwa kutumia kanuni ya uwiano-dhima, kithimu hicho ni yambwa$_{\varnothing}$ kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (5). Ni yambwa$_{\varnothing}$ badala ya yambwa, kwa sababu kinahusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki ya kithimu. Pia, licha ya kutokea katika nafasi ya yambwa na kuwa na mfungamano wa kimatamshi na kitenzi, hakiwezi kuwekewa kiambishi yambwa (**Angani kume**li**tanda* ***wingu zito***) au kuwa kiima cha sentensi tendwa (****Wingu zito*** *limetandwa na angani*).

**Kielelezo Na. 5:** ***Angani kumetanda wingu zito***

| | | |
|---|---|---|
| | *tanda* (<kithimu, kimahali>) | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui: | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima: | | [-h] |
| | Yambwa$_{\varnothing}$ | Kiima |

Kielelezo Na. (5) kinaonesha kuwa katika tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *tanda*, kimahali ni kiima na kithimu ni yambwa$_{\varnothing}$. Lugha ya Kiswahili inafanana na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kizulu (S40) na Kitharaka (E54). Katika lugha hizo, kitenzi chenye muundo huu kinakubali utokeaji wa upinduzi wa kimahali.

#### 4.2.1.2 Kitenzi chenye Muundo wa Mtenda, Kithimu na Kimahali (Tendwa)

Hiki ni kitenzi ambacho kiasili kina mtenda, kithimu na kimahali, lakini mtenda ameondolewa baada ya kuambikwa kiambishi cha utendwa -*w*-. Baada ya kuondolewa kwa mtenda, muundo wa kitenzi unabakiwa na kithimu pamoja na kimahali. Mifano ya vitenzi hivi ni *pambwa*, *pandwa*, *wekwa*, *achwa*, *pakwa*,

*atikwa*, *chorwa*, *fichwa*, *fagiwa*, *pangwa*, *chimbwa*, *mwagwa*, na *bandikwa*. Vitenzi hivi vinaruhusu upinduzi wa kimahali kama ilivyo katika mfano wa (10c).

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (10) | a) | *Anna* | ***a-me-pamb-a*** | *ma-ua* | *kanisa-ni* |
| | | kng1.Anna | kk1-knj-pamb-kt | kng6-ua | 5.kanisa-ktm |

‘Anna amepamba maua kanisani.’

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| b) | *Ma-ua* | ***ya-me-pamb-w-a*** | *kanisa-ni* | *(na Anna)* |
| | kng6-ua | 6-knj-pamb-ktndw-kt | 5-kanisa-ktm | (na Anna) |

‘Maua yamepambwa kanisani (na Anna).’

| | | | |
|---|---|---|---|
| c) | *Kanisa-ni* | ***ku-me-pamb-w-a*** | *ma-ua* |
| | kng5.kanisa-ktm | 17-knj-pamb-ktndw-kt | kng6-ua |

‘Kanisani kumepambwa maua.’

Katika mfano wa (10a), kitenzi ‘*pamba*’ kina mtenda *Anna*, kithimu *maua*, na kimahali *kanisani*. Katika mfano wa (10b), mchakato wa kimofosintaksia wa uambikaji wa kiambishi cha utendwa, umeondoa mtenda katika muundo wa kitenzi *pambwa*. Baada ya kuondolewa kwa mtenda, kitenzi kinabakiwa na kithimu pamoja na kimahali.

Aidha, katika tungo ya (10b), kwa kutumia kanuni ya kiima kwamba kila tungo lazima iwe na kiima, kithimu *maua* ni kiima na kimahali *kanisani* ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (6):

**Kielelezo Na. 6:** ***Maua yamepambwa kanisani***

| | *pambwa* <kithimu, kimahali> | |
|---|---|---|
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-h] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (6) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *pambwa*, kithimu ni kiima na kimahali ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$.

Kitenzi *pambwa* kinaruhusu utokeaji wa tungo yenye upinduzi wa kimahali (10c). Katika tungo hiyo, kwa kuzingatia kanuni ya kiima kwamba kila tungo lazima iwe na kiima, kimahali *kanisani* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima na kithimu *maua* kinashushwa hadhi na kuwa yambwa$_{\emptyset}$ kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (7). Kithimu hicho ni yambwa$_{\emptyset}$ badala ya yambwa kwa sababu hakiwezi kuwekewa kiambishi yambwa katika kitenzi (**Kanisani kume**ya**pambwa maua*).

**Kielelezo Na. 7:** ***Kanisani kumepambwa maua***

| | | |
|---|---|---|
| | *pambwa* (<kithimu, kimahali>) | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | | [-h] |
| | Yambwaø | Kiima |

Kielelezo Na. (7) kinaonesha kuwa katika tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *pambwa*, kimahali ni kiima na kithimu ni yambwaø.

### 4.2.2 Vitenzi Visivyoruhusu Upinduzi wa Kimahali
Licha ya vitenzi vinavyoruhusu upinduzi wa kimahali, lugha ya Kiswahili pia ina vitenzi visivyoruhusu upinduzi wa kimahali.

#### 4.2.2.1 Kitenzi chenye Muundo wa Mtenda na Kimahali cha Hiari
Hiki ni kitenzi ambacho muundo wake una mtendaji wa kitendo (mtenda). Licha ya kuwa na mtenda pia huweza kuambatana na kimahali cha hiari. Kitenzi chenye muundo huu huweza kuwa jongezi, tuli au cha uondoaji. Vitenzi hivi vyote haviruhusu upinduzi wa kimahali.

**(a) Kitenzi Jongezi chenye Muundo wa Mtenda na Kimahali cha Hiari**
Hiki ni kitenzi chenye mtenda pamoja na kimahali. Kitenzi hiki kinaonesha ujongeaji wa mtendaji wakati wa utendaji wa tendo. Kwa sababu mtenda anajongea, basi anaonesha pia mabadiliko ya mahali na hivyo anadhihirisha sifa za kithimu. Mifano ya vitenzi hivi ni *ruka*, *kimbia*, *tambaa*, *ogelea* na *zunguka*. Vitenzi hivi haviruhusu upinduzi wa kimahali kama inavyoonekana katika mfano wa 11(b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (11) | a) | *M-toto* | ***a-na-ruk-a*** | *ki-wanja-ni* |
| | | kng1-toto | kk1-knj-ruka-kt | kng7-kiwanja-ktm |
| | | 'Mtoto anaruka kiwanjani.' | | |
| | b) | **Ki-wanja-ni* | ***ku-na-ruk-a*** | *m-toto* |
| | | kng7-kiwanja-ktm | kk17-knj-ruka-kt | kng1-toto |
| | | '*Kiwanjani kunaruka mtoto.' | | |

Mfano wa (11a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Mfano wa (11b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *ruka*. Muundo wa kitenzi hiki una mtenda *mtoto* pamoja na kimahali cha hiari *kiwanjani*.

Katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali (11a), kwa kutumia kanuni ya kiima, mtenda *mtoto* ni kiima. Kwa sababu kuna kiima na kwa kuzingatia kanuni ya uwiano-dhima kwamba kila dhima moja ya kisemantiki ihusishwe na dhima moja

ya kisarufi na kinyume chake, kimahali cha hiari *kiwanjani* kinahusishwa na oblikyu$_{kimahali}$, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (8).

**Kielelezo Na. 8:** ***Mtoto anaruka kiwanjani***

| | *ruka* <mtenda, (kimahali)> | |
|---|---|---|
| | mtenda | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-h] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{kimahali}$ |

Kielelezo Na. (8) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *ruka*, mtenda ni kiima na kimahali cha hiari ni oblikyu$_{kimahali}$.

Katika tungo (11b), haiwezekani kutokea kwa upinduzi wa kimahali kwa sababu kuna mtenda *mtoto*. Mtenda yuko katika nafasi ya juu zaidi kuliko kimahali katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Iwapo kimahali *kiwanjani* kinapandishwa hadhi kuwa kiima, basi kunatokea tungo isiyokubalika kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (9).

**Kielelezo Na. 9:** ****Kiwanjani kunaruka mtoto***

| | *ruka* <mtenda, (kimahali)> | |
|---|---|---|
| | mtenda | (kimahali) |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | | *[-h] |
| | | Kiima |

Kielelezo Na. (9) kinaonesha kuwa uhusishaji wa kimahali *kiwanjani* na dhima ya kiima katika tungo ambayo imeundwa na kitenzi *ruka*, huzalisha tungo isiyokubalika.

**(b) Kitenzi Tuli chenye Muundo wa Mtenda na Kimahali cha Hiari**

Hiki ni kitenzi ambacho muundo wake una mtenda. Aidha, kitenzi hiki kinaweza kuambatana na kimahali cha hiari. Tofauti na mtenda katika kitenzi cha sehemu 4.3.1.1, mtenda katika kitenzi hiki hana sifa ya ujongezi, na kwa hiyo, hadhihirishi mabadiliko ya mahali. Mifano ya vitenzi hivi ni *nong'ona*, *tabasamu*, *koroma*, *cheka*, *sinzia*, *nguruma*, *lia* na *sikitika*. Vitenzi hivi haviruhusu upinduzi wa kimahali, kama inavyoonekana katika mfano wa (12b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (12) | a) | *M-gonjwa* | ***a-na-korom-a*** | *wodi-ni* |
| | | kng1-gonjwa | kk1-knj-koroma-kt | kng9.wodi-ktm |

'Mgonjwa anakoroma wodini.'

b) **Wodi-ni* ***ku-na-korom-a*** *m-gonjwa*
kn9-wodi-ktm kk17-knj-koroma-kt kng1-gonjwa
'*Wodini kunakoroma mgonjwa.'

Mfano wa (12a) unaonesha tungo isiyo ya upinduzi wa kimahali. Mfano wa (12b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *koroma*. Kitenzi *koroma* kina mtenda *mgonjwa* na kimeambatana na kimahali cha hiari *wodini*.

Katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali (12a), kwa kutumia kanuni ya kiima, mtenda *mgonjwa* ni kiima. Ni kiima kwa sababu yupo katika nafasi ya juu katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Kwa sababu kuna kiima, na kwa kuzingatia kanuni ya uwiano-dhima, kimahali cha hiari *wodini* kinahusishwa na oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (10). Ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ kwa sababu kinahusishwa na dhima ya kisemantiki ya kimahali. Pia, hakina sifa za yambwa kama vile kuwekewa kiambishi yambwa katika kitenzi (**Mgonjwa ana**ku**koroma **wodini***) au kuwa kiima cha sentensi tendwa (*****Wodini** kunakorom**wa** na mgonjwa*).

**Kielelezo Na. 10:** ***Mgonjwa anakoroma wodini***

| | | |
|---|---|---|
| | *koroma* <mtenda, (kimahali)> | |
| | mtenda | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-h] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (10) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *koroma*, mtenda ni kiima na kimahali cha hiari ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$.

Katika mfano wa (12b) haiwezekani kutokea kwa upinduzi wa kimahali kwa sababu kuna mtenda *mgonjwa* ambaye yuko katika nafasi ya juu zaidi kuliko kimahali katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Iwapo kimahali cha hiari *wodini* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima, kunatokea tungo isiyokubalika kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (11).

**Kielelezo Na. 11** ****Wodini kunakoroma mgonjwa***

| | | |
|---|---|---|
| | *koroma* (<mtenda, (kimahali cha hiari)>) | |
| | mtenda | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | | [-y] |
| | | Kiima |

Kielelezo Na. (11) kinaonesha kuwa uhusishaji wa kimahali cha hiari *wodini* na dhima ya kiima katika tungo ambayo imeundwa na kitenzi *koroma*, huzalisha tungo isiyokubalika.

**(c) Kitenzi cha Uondoaji chenye Muundo wa Mtenda na Kimahali cha Hiari**

Kitenzi hiki kinaonesha utoaji wa kitu kutoka ndani kwenda nje ya mwili. Kitenzi hiki kinahitaji mtoaji wa kitu na kitu kinachotolewa, ambacho siyo lazima kitajwe. Aidha, kitenzi hiki kinaweza kuambatana na kimahali cha hiari. Mifano ya vitenzi hivi ni *kojoa*, *kunya*, *harisha*, *sukutua* na *tapika*. Vitenzi hivi haviruhusu upinduzi wa kimahali, kama ilivyo katika mfano wa (13b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (13) | a) | *M-toto* | ***a-me-kojo-a*** | *bafu-ni* |
| | | kng1-toto | kk1-knj-kojo-kt | kng5.bafu-ktm |
| | | 'Mtoto amekojoa bafuni.' | | |
| | b) | **Bafu-ni* | ***ku-me-kojo-a*** | *m-toto* |
| | | kng5.bafu-ktm | kk17-knj-kojo-kt | kng1-toto |
| | | '*Bafuni kumekojoa mtoto.' | | |

Mfano wa (13a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Mfano wa (13b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *kojoa*. Muundo wa kitenzi hiki una mtenda *mtoto* pamoja na kimahali cha hiari *bafuni*.

Katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali, mtenda *mtoto* ni kiima kwa sababu yupo katika nafasi ya juu katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Kwa sababu kuna kiima na kwa kuzingatia kanuni ya uwiano-dhima, kimahali cha hiari, *bafuni* ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (12).

**Kielelezo Na. 12:** ***Mtoto anakojoa bafuni***

| | | |
|---|---|---|
| | *kojoa* <mtenda, (kimahali)> | |
| | mtenda | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-h] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (12) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *kojoa*, mtenda ni kiima na kimahali cha hiari ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$. Katika mfano wa (13b) haiwezekani kutokea kwa upinduzi wa kimahali kwa sababu kuna mtenda *mtoto* ambaye yuko katika nafasi ya juu kuliko kimahali katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Iwapo kimahali, *bafuni* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima, kunatokea tungo isiyokubalika kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (13).

**Kielelezo Na. 13:** ***Bafuni kunakojoa mtoto***

| | | |
|---|---|---|
| | *kojoa* <mtenda, (kimahali cha hiari)> | |
| | mtenda | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | | [-y] |
| | | Kiima |

Kielelezo Na. (13) kinaonesha kuwa uhusishaji wa kimahali cha hiari *bafuni* na dhima ya kiima katika tungo ambayo imeundwa na kitenzi *kojoa*, huzalisha tungo isiyokubalika.

#### 4.2.2.2 Kitenzi chenye Muundo wa Mtenda, Kithimu na Kimahali (Tenda)

Hiki ni kitenzi mahali ambacho kina muundo wake una mtenda, kithimu na kimahali. Mifano ya vitenzi hivi ni *panda*, *weka*, *acha*, *paka*, *atika*, *chora*, *ficha*, *fagia*, *panga*, *chimba*, *mwaga* na *bandika*. Vitenzi hivi haviruhusu upinduzi wa kimahali kama ilivyo katika mfano wa (14b).

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (14) | a) | *Anna* | ***a-me-wek-a*** | *vi-kombe* | *kabati-ni* |
| | | kng1.Anna | kk1-knj-wek-kt | kng8-kikombe | 5.kabati-ktm |
| | | 'Anna ameweka vikombe kabatini.' | | | |
| | b) | **Kabati-ni* | ***ku-me-wek-a*** | *vi-kombe* | *Anna* |
| | | kng5.kabati-ktm | kk17-knj-wek-kt | kng17-knj-wek-kt | kng1-Anna |
| | | 'Kabatini kumeweka vikombe Anna.' | | | |

Mfano wa (14a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Mfano wa (14b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *weka*. Muundo wa kitenzi hiki una mtenda *Anna*, kithimu *vikombe*, na kimahali *kabatini*.

Katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali, kwa kutumia kanuni ya kiima mtenda *Anna* anahusishwa na kiima kwa sababu yupo katika nafasi ya juu katika udarajia wa dhima za kisemantiki. Kwa sababu kuna kiima, na kwa kuzingatia kanuni ya uwiano-dhima, kithimu *vikombe* ni yambwa na kimahali *kabatini* ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$, kama ilivyo katika kielelezo Na. (14).

**Kielelezo Na. 14:** ***Anna ameweka vikombe kabatini***

| | | | |
|---|---|---|---|
| | *weka* <mtenda, kithimu, kimahali> | | |
| | Mtenda | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-h] | [+y] | [+h] |
| | Kiima | Yambwa | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (14) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *weka*, mtenda ni kiima, kithimu ni yambwa, na kimahali ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$.

Kwa sababu kuna mtenda na kithimu, na kwa kuwa mtenda yupo katika nafasi ya juu katika udarajia wa dhima za kisemantiki kuliko kithimu, hakuna mazingira ya uhusishaji wa kimahali *kabatini* na dhima ya kiima. Iwapo kimahali *kabatini* kinapandishwa hadhi kuwa kiima, basi kunatokea tungo isiyokubalika, kama ilivyo katika kielelezo Na. (15). Kitenzi hiki kinaruhusu upinduzi wa kimahali iwapo mtenda anaondolewa kwa kutumia mchakato wa utendwa kama ilivyofafanuliwa katika sehemu 4.2.1.2.

**Kielelezo Na. 15:** ***Kabatini mumeweka vikombe Anna***

| | | | |
|---|---|---|---|
| | *weka* <mtenda, kithimu, kimahali> | | |
| | Mtenda | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-y] | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | | | *[-h] |
| | | | Kiima |

Kielelezo Na. (15) kinaonesha kuwa uhusishaji wa kimahali *kabatini* na dhima ya kiima katika tungo ambayo imeundwa na kitenzi *weka*, huzalisha tungo isiyokubalika.

Kwa ujumla, muhtasari wa vitenzi vinavyoruhusu na visivyoruhusu upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili umeoneshwa katika Jedwali Na. (1). Katika jedwali hilo vitenzi vinavyoruhusu vimewekewa alama ya √ na vile visivyoruhusu vimewekewa alama ya ×:

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Vitenzi Vinavyoruhusu na Visivyoruhusu Utokeaji wa Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili**

| # | Aina ya Kitenzi | Muundo wa Vishiriki vya Kitenzi | Kinaruhusu |
|---|---|---|---|
| **1** | **Kitenzi ambacho kina kithimu na kimahali** | | |
| a | Kitenzi jongezi chenye kithimu na kimahali | <kithimu, kimahali> | √ |
| b | Kitenzi tuli chenye kithimu na kimahali | <kithimu, kimahali> | √ |
| **2** | **Kitenzi ambacho kina mtenda, kithimu, na kimahali** | | |
| a | Kitenzi chenye mtenda, kithimu, na kimahali (Tendwa) | <kithimu, kimahali> | √ |
| **3** | **Kitenzi ambacho kina mtenda na kimahali** | | |
| a | Kitenzi jongezi chenye mtenda na kimahali cha hiari | < mtenda, (kimahali)> | × |
| b | Kitenzi tuli chenye mtenda na kimahali cha hiari | < mtenda, (kimahali)> | × |

| | | | |
|---|---|---|---|
| c | Kitenzi cha uondoaji chenye mtenda na kimahali cha hiari | <mtenda, (kimahali)> | × |
| **4** | **Kitenzi ambacho kina mtenda, kithimu, na kimahali** | | × |
| a | Kitenzi chenye mtenda, kithimu, na kimahali (Tenda) | <mtenda, kithimu, kimahali> | × |
| | | | |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Kwa ujumla, sehemu 4.2 imebainisha vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu upinduzi wa kimahali. Imebainika kwamba kitenzi kinachoruhusu upinduzi wa kimahali lazima kiwe na muundo wa kithimu na kimahali. Iwapo kitenzi kina mtenda, kithimu na kimahali; lazima mtenda aondolewe kwa uambikaji wa kiambishi cha utendwa -*w*-. Aidha, kitenzi chenye mtenda katika muundo wake, hakiruhusu upinduzi wa kimahali. Baada ya sehemu hii, sehemu inayofuata inahusu vimahali vinavyoweza na vile visivyoweza kupinduliwa katika tungo.

### 4.3 Vimahali Vinavyoweza na Vile Visivyoweza Kupinduliwa

De Armond na Hedberg (2002) wanaeleza kwamba kuna viambajengo vya aina tatu katika tungo. Viambajengo hivyo ni kijalizo cha msingi, chagizo, na kiambajengo kilicho katika mpaka wa kijalizo cha msingi na chagizo. Vimahali kama viambajengo vingine vya sentensi huweza kuangukia katika makundi haya. Hata hivyo, katika makala hii, vimahali vimeainishwa katika makundi mawili; yaani, vijalizo na chagizo. Sehemu zinazofuata tumebainisha vimahali vinavyoweza kupinduliwa na vile visivyoweza kupinduliwa.

#### 4.3.1 Vimahali Vinavyoweza Kupinduliwa

Imebainika kwamba vimahali vinavyoweza kupinduliwa ni vijalizo. Kijalizo ni kipashio kinachokamilisha maana katika tungo. Aidha, kipashio hiki ni cha lazima na hakiwezi kuondolewa bila kuleta athari ya kisarufi. Vimahali huweza kuwa vijalizo kwa namna mbili. Kwanza, ni vijalizo vya kitenzi mahali kama ilivyo katika mfano wa (3a). Hivi ni vishiriki katika miundo ya vishiriki vya kitenzi. Pili, vijalizo vya kiambishi cha utendea kama ilivyo katika mfano wa (3b). Hivi vimetokana na uambikaji wa kiambishi cha utendea.

##### 4.3.1.1 Vijalizo vya Kitenzi Mahali

Hivi ni vimahali ambavyo vinakamilisha maana katika miundo ya vishiriki vya kitenzi. Vimahali hivi hujaliza kitenzi mahali kama vile *ingia*, *toka*, *enea*, *zagaa*, *tanda*, *paka*, *ondoa*, *weka* na *panga*. Vimahali hivi huweza kupinduliwa kama inavyoonekana katika mfano wa 15(b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (15) | a) | *Taka* | *zi-me-zaga-a* | ***sakafu-ni*** |
| | | kng10.taka | kk10-knj-zaga-kt | kng9.sakafu-ktm |

‘Taka zimezagaa sakafuni.’

| | | | |
|---|---|---|---|
| b) | ***Sakafu-ni*** | *pa-me-zaga-a* | *taka* |
| | kng9.sakafu-ktm | kk16-knj-zaga-kt | kng10.taka |
| | ‘Sakafuni pamezagaa taka.’ | | |

Mfano wa (15a) unaonesha tungo isiyo ya upinduzi wa kimahali. Mfano wa (15b) unaonesha tungo yenye upinduzi ambapo kimahali *sakafuni* kimepinduliwa. Tungo hizi zimeundwa na kitenzi *zagaa*. Muundo wa kitenzi hiki una kithimu *taka* na kimahali *sakafuni*. Kwa hiyo, kimahali *sakafuni* ni kijalizo na kinakamilisha muundo wa semantiki wa kitenzi.

Katika tungo isiyo na upinduzi, kwa kutumia kanuni ya kiima kithimu *taka* kinahusishwa na kiima na kimahali *sakafuni* kinahusishwa na oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. (16).

**Kielelezo Na. 16:** ***Taka zimezagaa sakafuni***

| | | |
|---|---|---|
| | *zagaa* <thimu, kimahali> | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | [-y] | [+h] |
| | Kiima | Oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$ |

Kielelezo Na. (16) kinaonesha kuwa katika tungo isiyo na upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi *zagaa*, kithimu ni kiima na kimahali ni oblikyu$_{\textbf{kimahali}}$.

Katika tungo yenye upinduzi, kimahali *sakafuni* kinapandishwa hadhi na kuwa kiima, na kithimu *taka* kinashushwa hadhi na kuwa yambwa$_{\textbf{kithimu}}$ kama ilivyo katika kielelezo Na. (17):

**Kielelezo Na. 17:** ***Kiwanjani pamezagaa taka***

| | | |
|---|---|---|
| | *zagaa* <thimu, kimahali> | |
| | kithimu | kimahali |
| Uhusishaji kimajumui | [-h] | [-y] |
| Uhusishaji kiima | | [-h] |
| | Yambwa$_{ø}$ | Kiima |

Kielelezo Na. (17) kinaonesha kuwa katika tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo imeundwa na kitenzi z*agaa*, kithimu ni yambwa$_{ø}$ na kimahali ni kiima.

### 4.3.2 Vimahali Visivyoweza Kupinduliwa

Imebainika kwamba vimahali visivyoweza kupinduliwa ni chagizo. Chagizo ni kiambajengo cha hiari katika tungo. Kiambajengo hiki huweza kuondolewa bila kuleta athari ya kisarufi katika tungo. Vimahali ambavyo ni chagizo huambatana na vitenzi visivyohitaji kujalizwa na kimahali. Mathalani, vimahali vinavyoambatana na vitenzi *koroma*, *ongea*, *nong’ona*, *imba*, *cheka*, *lia*, *sali* na

*kula*. Vimahali hivi haviwezi kupinduliwa kama inavyoonekana katika mfano wa (16b).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (16) | a) | *M-toto* | *a-na-li-a* | ***nyumba-ni*** |
| | | kng1-toto | kk1-knj-li-kt | kng9.nyumba-ktm |
| | | 'Mtoto analia nyumbani.' | | |
| | b) | ****Nyumba-ni*** | *ku-na-li-a* | *m-toto* |
| | | kng9.nyumba-ktm | kk17-knj-li-kt | kng3-toto |
| | | 'Nyumbani kunalia mtoto.' | | |

Mfano wa (16a) unaonesha tungo isiyo ya upinduzi wa kimahali. Mfano wa (16b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki. Tungo hii imeundwa na kitenzi *analia* ambacho kinahitaji mtenda tu. Aidha, kimahali *nyumbani* ni chagizo na hivyo hakiwezi kupinduliwa. Uhusishaji wa kimahali *nyumbani* na kiima huzalisha tungo isiyokubalika.

## 5.0 Hitimisho

Kwa ujumla, upinduzi wa kimahali ni mchakato unaojidhihirisha katika lugha ya Kiswahili. Tofauti na lugha nyingi za Kibantu ambazo hudhihirisha upinduzi wa kimahali wa kimofolojia au wa kisemantiki, lugha ya Kiswahili ina aina zote mbili za upinduzi wa kimahali. Aidha, kuna vitenzi ambavyo vinaruhusu utokeaji wa mchakato huo. Vitenzi hivyo lazima viwe na kithimu pamoja na kimahali ambacho ni kijalizo. Kwa upande mwingine kuna vitenzi ambavyo haviruhusu utokeaji wa mchakato huo. Vitenzi hivyo ni vile ambavyo vina mtenda katika muundo wake. Vilevile, vimahali vinavyoweza kupinduliwa ni vijalizo. Kwa upande mwingine, vimahali visivyoweza kupinduliwa ni chagizo.

## Marejeleo


Amidu, A.A. (2007). Why Locative Marking in Kiswahili Bantu is not that Simple, *The Linguistic Association of Korean Journal*, 15 (3): 21- 42.

Bresnan, J. (1994). Locative Inversion and Architecture of Universal Grammar, *Language*, 70: 72 - 131.

Bresnan, J. and Kanerva, J.M. (1989). Locative Inversion in Chichewa: A Case Study of Factorization in Grammar, *Linguistic Inquiry*, 20: 1- 50.

Bresnan, J. and Kaplan, R.M. (1982). Introduction: Grammars as Mental Representation of Language, in J. Bresnan (ed.), *The Mental Representation of Grammatical Relations*, Cambridge, MA: The MIT Press, pp. xvii – xviii.

Buberwa, A. (2016). Mofolojia ya Majina ya Mahali ya Kiswahili na Kihaya katika Jamii ya Wahaya: Uzingativu wa Masuala ya Kiisimu Jamii. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Buel, L. (2007). Semantic and Formal Locatives: Implications for the Bantu Locative Inversion Typology, *SOAS Working Papers in Linguistics*, 15: 105 - 120.

Creissels, D. (2011). Tswana Locatives and their Status in Inversion Construction, *Africana Linguistica*, 17: 33 - 52.

Demuth, K. and Mmusi, S. (1997). Presentational Focus and Thematic Structure in Comparative Bantu, *Journal of African Languages and Linguistics*, 18:1 - 19.

Diercks, M. (2009). The Morphostyntax of Lubukusu Locative Inversion and Parameterization of Agreement, *Lingua*, 121: 702 - 720.

Givon, T. (2001). *Syntax*: Vol. I & II. Amsterdam: John Benjamins.

Guérois, H. (2016). The Locative System in Cuwabo and Makhuwa (P30 Bantu Languages), *African Languages and Linguistics*, 2: 43-76.

Harford, C. (1990). Locative Inversion in Chishona, in J. Hutchison and V. Manfredi (eds.), *Current Approaches to African Linguistics*, Dodretch: Foris, pp. 137 - 144.

Kim, M. (1999). A Cross-Linguistic Perspective on the Acquisition of Locative Verbs. PhD Dissertation, University of Delaware.

Kroeger, P.R. (2004). *Analysing Syntax: Alexical Functional Approach*. Cambaridge: Cambaridge University Press.

Marten, L. (2006). Locative Inversion in Otjiherero: More on Morphostntactic Variation in Bantu, *ZAS Papers in Linguistics African Linguistics*, 43: 97 - 122.

Marten, L. and Van der Wal, J. (2014). A Typology of Bantu Subject Inversion, *Linguistic Variation*, 14-2: 318 - 368.

Marten, L. (2013). Structure and Interpretation in Swahili Existential Constructions, *Rivista di Linguistica*, 25(1): 45 - 73.

Mkude, D. J. (2005). *The Passive Construction in Swahili*, Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Mpiranya, F. (2015). *Swahili Grammar Workbook*. London: Taylor and Francis Group.

Polomé, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington: Center for Applied Linguistics.

Salzman, M. D. (2011). Towards a Typology of Locative Inversion- Bantu, Perhaps Chinese and English-But Beyond?, *Language and Linguistics Compass*, 1- 21.

Salzmann, M. D. (2004). *Theoretical Approaches to Locative Inversion*. MA Dissertation, University of Zurich.

Zeller, J. (2013). Locative Inversion in Bantu and Predication, *Linguistics*, 51(6): 1107- 1146.

## Alama na Vifupisho Vilivyotumika

| | | |
|---|---|---|
| kk | = | kipatanishi cha kiima |
| kng | = | kiambishi ngeli |
| knj | = | kiambishi njeo |
| kt | = | kiambishi tamati |
| ktm | = | kiambishi tamati mahali |
| ky | = | kiambishi yambwa |
| ktnda | = | kiambishi tendea |
| ktndw | = | kiambishi tendwa |
| * | = | Kiambishi ambacho ni Mame-Bantu |
| * | = | Tungo isiyokubalika |
| < > | = | Muundo vishiriki vya kitenzi |
| <( x )> | = | Kipashio x ni kishiriki cha hiari katika muundo wa vishiriki vya kitenzi |